



SYRACUSE CITY SCHOOL DISTRICT
Jaime Alicea, Msimamizi wa Shule

Ofisi ya Msimamizi

Alhamisi, 9 Aprili 2020

Kwa Familia,

Kama nilivyoripoti mapema wiki hii, New York State Board of Regents na State Education Department zilitangaza ufutiliaji mbali wa mitihani ya Regents ya Juni 2020. Sasa tuna mwongozo wa ziada wa kushiriki nawe kuhusu maana ya suala hili kwa wanafunzi.

New York State Department of Education imebadilisha matakwa ili wanafunzi wote ambao wamesajiliwa kwa sasa katika madaraja ya 7-12, wakiwemo wa mwaka wa mwisho, waliokuwa wakikusudia kushiriki katika mtihani wa Regents Juni hii wanastahiki kutojumuishwa kwenye mitihani hiyo.

Wanafunzi watastahiki kupokea alama za NYS Diploma bila kufanya na hawatahitajika kufanya mtihani wa Regents chini ya hali zifuatazo:

- Mwanafunzi amesajiliwa kwa sasa katika kozi ya kiwango cha Regents au alikuwa amesajiliwa awali katika kozi hiyo.
- Mwanafunzi amepita au hupita kozi ya kiwango cha Regents mwaka huu na anapokea alama za kozi.
- Mwanafunzi alikuwa akikusudia kufanya mtihani wa Regents wa kozi Juni hii.
- Mwanafunzi alikuwa amesajiliwa katika kozi ya kiwango cha Regents, hakupokea alama za kozi na anahuduria mafunzo ya shule ya majira ya joto na kupita kozi kwa alama katika mwezi wa Agosti 2020.

Pia nilitaka kuwafahamisha kuwa tunakamilisha matakwa ya kuweka madaraja kwa kipindi cha kusahihisha cha robo ya nne. Tutashiriki taarifa za ziada hivi karibuni suala hili likirasimishwa. Kwa wanafunzi ambao huenda wakahitaji muda wa ziada kukamilisha na kuwasilisha kazi, walimu wanaweza kuweka Incomplete (I) ili kuruhusu muda zaidi wa kufanya kazi kwa nyakati hizi zisizobainika.

Ninashukuru uelewa na usaidizi wenu tunapo jitahidi kuwapasha habari katika hali hizi zinazobadilika.

Tafadhali endeleeni kuwa salama,

A handwritten signature in black ink that reads "Jaime Alicea".

Jaime Alicea
Msimamizi wa Shule